

# Fatuma anaenda sokoni

## Swahili

Siku moja asubuhi Fatuma aliamshwa na mama yake alivyokuwa amelala na akasema "Fatuma leo tunaenda sokoni, inabidi tuondoke kabla joto halijazidi huko nje. Kwahiyo njoo kunywa uji na tuondoke".

Fatuma alifanya haraka sana kuvaa nguo na kunywa uji wake ili aweze kwenda sokoni na mama yake. Fatuma alipenda sana kwenda sokoni.

Ili kufika sokoni ilibidi kwanza kupanda basi. Kwa bahati nzuri safari ilikuwa ni fupi tu na walivyofika mama Fatuma alilipia safari na wakashuka.

Fatuma anapenda sana kwenda sokoni kwasababu kuna harufu nyingi nzuri na sauti mbali mbali na vitu vingi sana vya kuangalia.

Kitu cha kwanza wanachonunua leo ni tikiti maji. Mama Fatuma anajua sana jinsi ya kuchagua tikiti maji lililoiva kwa kuligonga na mkono. Pamoja wananunua tikiti maji zuri na tamu sana.

Baada ya hapo wananunua nyanya, vitunguu na karoti. Wanavipata vyote kwa bei nzuri na wanalipia.

Pembeni mwa soko kuna fundi cherehani anaye tengeneza nguo. Fatuma anaenda kuchagua gauni zuri sana ambalo fundi cherehani amemtengenezea. Fatuma anapenda sana kwenda kwa fundi cherehani kwasababu kuna nguo nzuri na vitambaa vizuri sana vya kuangalia.

Baada ya kuondoka kwa fundi cherehani kuna kitu kimoja tu zaidi cha kufanya. Wanarudi tena ndani ya soko kwenye eneo lenye wanyama kama kuku na mbuzi. Mama yake Fatuma ananunua mayai ya kuku halafu wote wawili wanarudi nyumbani.

Siku hii ilikuwa nzuri sana na Fatuma pia amefurahi sana.

# Fatuma anaenda sokoni

## English

One day Fatuma was woken up by her mother while she was asleep and said, "Fatuma today we are going to the market, we have to leave before it gets too hot outside. So come and have your porridge so we can leave."

Fatuma hurried up to get dressed and to have her porridge so that she could go to the market with her mother. Fatuma really likes going to the market.

To get to the market you had to take the bus. Luckily the ride was short and when they arrived Fatuma's mom paid for the ride and they got off.

Fatuma likes going to the market because there are a lot of nice smells and many different sounds and a lot of things to look at.

The first thing they buy today is a watermelon. Fatuma's mom is good at choosing ripe watermelons by tapping them with her hand. Together they buy a nice and tasty watermelon.

After that they buy tomatoes, onions and carrots. They get all of this for a good price and they pay for it.

Next to the market there is a tailor who makes clothes. Fatuma goes to choose a very nice dress that the tailor has made for her. Fatuma likes going to the tailor very much because there are nice clothes and fabrics to look at.

After leaving the tailor there is only one more thing to do. They go back into the market to the area where there are animals such as chicken and goats. Fatuma's mom buys chicken eggs and then they both head back home.

This was a really nice day and Fatuma is also really happy.